



دعوت اسلامی کا تعارف

U
T
A
N
G
U
L
I
Z
I
W
A

Dawat-e-Islami

(Swahili)



مکتبۃ الدین
Dawat-e-Islami

Presented by:
Markazi Majlis-e-Shura

دَعْوَتِ اِسْلَامِي كَا تَعَارُف

Utangulizi wa DAWAT-E-ISLAMI

Umewasilishwa na

Markazi Majlis-e-Shura

Translation Majlis (Dawat-e-Islami)

Alami Madani Markaz, Faizan-e-Madina, Mahalla Saudagran,
Old Sabzi Mandi, Baab-ul-Madina, Karachi, Pakistan

Contact #: +92-21-34921389 hadi 91

translation@dawateislami.net

الْحَمْدُ لِلَّهِ رَبِّ الْعَالَمِينَ وَالصَّلَاةُ وَالسَّلَامُ عَلَى سَيِّدِ الْمُرْسَلِينَ
أَمَّا بَعْدُ فَأَعُوذُ بِاللَّهِ مِنَ الشَّيْطَانِ الرَّجِيمِ بِسْمِ اللَّهِ الرَّحْمَنِ الرَّحِيمِ ط

Dua Kabla Ya Kusoma Kitabu

Kabla ya kusoma kitabu au somo la kidini, soma dua ifuatayo.

إِنْ شَاءَ اللَّهُ عَزَّوَجَلَّ utakumbuka yote uliyoyasoma.

اللَّهُمَّ افْتَحْ عَلَيْنَا حِكْمَتَكَ وَأَنْشُرْ
عَلَيْنَا رَحْمَتَكَ يَا ذَا الْجَلَالِ وَالْإِكْرَامِ

Ee mola عَزَّوَجَلَّ Ifungue milango ya elimu na busara kwa ajili yetu, na utuhurumie! Ewe ulie mtakatifu kabisa. *(Al-Mustatraf Vol. I, P. 40, Dar-ul-Fikr, Beirut)*

Kumbuka: Mswalie Mtume صَلَّى اللهُ تَعَالَى عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ mara moja kabla na baada ya dua. *(Roohani Hikiyat UK. 68)*

Chati ya unukuu

ء	A/a	ژ	Ř/ř	ل	L/l
ا	A/a	ز	Z/z	م	M/m
ب	B/b	ژ	X/x	ن	N/n
پ	P/p	س	S/s		V/v,
ت	T/t	ش	Sh/sh	و	W/w
ٹ	Ĥ/ĥ	ص	Ş/ş	ه / ه / ة	Ĥ/ĥ
ث	Š/š	ض	Đ/đ	ی	Y/y
ج	J/j	ط	Ṭ/ṭ	ے	Y/y
چ	Ch	ظ	Ẓ/ẓ	َ	A/a
ح	Ĥ/ĥ	ع	‘	ُ	U/u
خ	Kh/kh	غ	Gh/gh	ِ	I/i
د	D/d	ف	F/f	و مدّه	Ū/ū
ڈ	Ḍ/ḍ	ق	Q/q	ی مدّه	Ī/ī
ذ	Ẓ/ẓ	ک	K/k	ا مدّه	Ā/ā

Orodha Ya Yaliyomo

Utangulizi wa_DAWAT-E-ISLAMI.....	1
Dua Kabla Ya Kusoma Kitabu	ii
Chati ya unukuu	iii
DAWAT-E-ISLAMI	1
Ubora Wa Kumswalia Mtume صَلَّى اللهُ تَعَالَى عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ	1
Umuhimu wa Dawat-e-Islami	2
Kila mmoja ni Mlinganizi	3
Kuasisiwa Dawat-e-Islami	3
Dawat-e- Islami katika Mataifa 176	5
Ulinganizi kati ya Wasio Waislamu	6
Kafiri Asilimu	6
Madani Qafilah.....	7
Nyuso Memetefu Zinasababisha Kusilimu	8
Vituo vya Masomo vya Madani.....	9
Kujenga Misikiti.....	9
Maimamu Wa Misikiti.....	10
Viziwi, Mabubu na Vipofu	10

Kafiri Asilimu	11
Ulinganizi Gerezani	12
Habusu Arekebishika.....	13
Itikaf ya Pamoja.....	15
Ijtimai kubwa baada ya Hajj.....	16
Mabadiliko ya KiMadani kwa Kina Dada wa Kiislamu	17
Mifano kidogo ya Shughuli za Mwezi za akina Dada.....	18
Tazama namna Mazingira ya KiMadani yanavyombadilisha mui kuwa mwema!	19
Madani In'āmāt.....	20
Bishara njema kwa wanaofuata Madanī In'āmāt	21
Madanī Muḏākaraḥ	22
Tiba ya Kiroho na Istikharah.....	22
Uvimbe wa Ubongo.....	23
Kuwafunza Mahujjaji.....	24
Taasisi za Ilimu	25
Jamiatul Madina.....	25
Madrasa-tul-Madīnaḥ	26
Madrasa-tul-Madīnaḥ (kwa watu wazima)	26
Kliniki.....	27
Takhaṣṣuṣ-fil-Fiqḥ.....	27
Majlis Taḥqīqāt-e-Shar'iyah.....	28

Dār-ul-Iftā Aĥl-e-Sunnat	28
Mtandao	29
Dār-ul-Iftā Aĥl-e-Sunnat katika Mtandao.....	29
Maktaba-tul-Madīnaĥ	29
Al-Madīna-tul-‘Ilmiyyaĥ	30
Majlis-e-Taftīsh Kutub-o-Rasāil	31
Kozi Mbalimbali.....	32
Īṣāl-e-Šawāb	32
Viduka vya Maktaba-tul-Madīnaĥ.....	32
Majlis-e-Tarājim	33
Ijtimāi Ng’ambo.....	33
Tarbiyyati Ijtimai	34
Madrasa-tul-Madīnaĥ Katika mtandao.....	34
Dār-ul-Madīnaĥ.....	34
Madanī Chaneli	35
1. Asiyekuwa Muislamu, anaukubali Uislamu	37
2. Sasa naona aibu kutazama idhaa zenye kuonyesha uchafu.....	38
3. Baa ilifungwa	39
Maua 8 ya Madani ya Dawat-e-Islami.....	39
Idara 63 za Dawat-e-Islami.....	48

الْحَمْدُ لِلَّهِ رَبِّ الْعَالَمِينَ وَالصَّلَاةُ وَالسَّلَامُ عَلَى سَيِّدِ الْمُرْسَلِينَ
أَمَا بَعْدُ فَأَعُوذُ بِاللَّهِ مِنَ الشَّيْطَانِ الرَّجِيمِ بِسْمِ اللَّهِ الرَّحْمَنِ الرَّحِيمِ ط

Utangulizi wa DAWAT-E-ISLAMI

Ijapokuwa shetani atakutia uvivu, tafadhali soma kijitabu hiki chote. **إِنْ شَاءَ اللَّهُ عَزَّوَجَلَّ** Utapata mabadiliko makubwa ya KiMadani katika moyo wako.

Ubora Wa Kumswalia Mtume ﷺ

Mtume mtukufu **صَلَّى اللَّهُ تَعَالَى عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ** amesema, Malaika Jibril **عَلَيْهِ السَّلَام** aliniambia ya kwamba Allah **عَزَّوَجَلَّ** anasema, “Ewe Muhammad! Hupendezewi na kwamba kila mfuasi wako akituma swala moja kwako, Mimi nitamteremshia rehema kumi juu yake, na akituma amani moja kwako wewe, Mimi nitamteremshia amani kumi kwake. (*Mishkāt-ul-Maṣābīh, Juz 1, uk. 189, Hadith na. 928*)

صَلَّى اللَّهُ تَعَالَى عَلَى مُحَمَّدٍ

صَلُّوا عَلَى الْحَبِيبِ

Umuhimu wa Dawat-e-Islami

Allah ﷻ anasema katika Qurani tukufu, Aya 104 ya Surah Al Imran:

وَلْتَكُنْ مِنْكُمْ أُمَّةٌ يَدْعُونَ إِلَى الْخَيْرِ وَيَأْمُرُونَ بِالْمَعْرُوفِ وَيَنْهَوْنَ
عَنِ الْمُنْكَرِ وَأُولَئِكَ هُمُ الْمُفْلِحُونَ ﴿١٠٤﴾

Na uwe kutokana na nyinyi umma unaolingania kheri na unaoamrisha mema na unakataza maovu. Na hao ndio waliofanikiwa.

(Āl 'Imrān, aya 104, qara 4)

Mufti Ahmad Yar Khan رَحْمَةُ الْخَانَ، mufassir mkubwa wa Qurani, akiisherehesha aya hii katika kitabu Tafsīr-e-Na'imī, Juzuu ya 4, uk. 72 amesema, Enyi Waislamu! Inatakiwa paweko na umma au kundi kama hili kati yenu na ikiwa hakuna basi hapana budi kuanzishwa kundi hili la kudumu lenye kuwalingania watu wabaya kwenye utakaso, wasiokuwa waislamu kwenye uislamu, madhalimu kwenye uongofu, walioghafilika kwenye kutanabahi, wajinga kwenye uwekevu na utambuzi, wakavu (wa imani) kwenye kujenga mapenzi ya dini na wenye utepetevu kwenye msimamo wa kidini.

Aidha, kundi hili lilinganie watu katika imani sahihi, tabia njema na matendo mema kwa kuhubiri, kuandika, kimatendo,

kiulainifu na kinguvu (mtawala kwa raia wake). Vile vile kundi hili liwazuie watu kutokana na imani potofu, tabia mbaya, matendo mabaya, nia chafu na fikra mbovu ima kwa ulimi, moyo, maandishi na hata kwa nguvu (kulingana na cheo cha mtu).

Kila mmoja ni Mlinganizi

Mufti huyu رَحْمَةُ اللَّهِ تَعَالَى عَلَيْهِ ameendelea kueleza, “Waislamu wote ni walinganizi. Ni faradhi (lazima) kwao kuwaamrisha watu kufanya matendo mema na kukataza kufanya maovu.” Maana yake ni kuwa kila muislamu ana jukumu la kufikisha akijuacho kwa waislamu wengine. Kulingana na hadithi ya Mtume mtukufu صَلَّى اللَّهُ تَعَالَى عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ aliposema:

بَلِّغُوا عَنِّي وَلَوْ آيَةً

“Nifikishieni kwa niaba yangu hata kama ni aya moja.” (*Sahih*

Bukhari, Juz. 2, uk. 462 Hadith 3461)

Kuasisiwa Dawat-e-Islami

Ndugu Waislamu! Katika kila karne, Allah عَزَّوَجَلَّ ametuma watu watukufu kwa umma wa Mtume Mtukufu صَلَّى اللَّهُ تَعَالَى عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ ambao wametekeleza wajibu wa: ‘أَمْرٌ بِالْمَعْرُوفِ وَنَهْيٌ عَنِ الْمُنْكَرِ’
Kuwaita watu kufanya mema na kuwakataza watu kutenda matendo mabaya. Mawalii hawa wamejenga fikra kwa

waislamu kwamba: “Nitajaribu kusuluhisha nafsi yangu na watu wa ulimwengu mzima.” *إِنْ شَاءَ اللَّهُ عَزَّوَجَلَّ*

Mmoja wa mabwana hawa ni Shaykh-e-Tarīqat Amīr-e-Ahl-e-Sunnat ‘Allāmah Maulānā Abu Bilal Muhammad Ilyas Attar Qadiri Razavi Ziyāee *دَامَتْ بَرَكَاتُهُمُ الْعَالِيَةِ* ambaye katika mfungo pili mwaka wa 1401H (September 1981) yeye na wenzake, walianzisha Dawat-e-islami (Shirika la Kimataifa la Kueneza Mafundisho ya Quran na Sunna lisilojihusisha na Siasa) katika mji wa Babul Madina (Karachi)

Amīr-e-Ahl-e-Sunnat *دَامَتْ بَرَكَاتُهُمُ الْعَالِيَةِ* ni kielelezo cha mawalii wa zamani katika kumcha Allah *عَزَّوَجَلَّ*, dhati ya kumpenda Mtume *صَلَّى اللَّهُ تَعَالَى عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ*, jazba ya kufuata Qur’an na sunnah, kuhuisha sunnah, uongofu, usamehevu, subira, shukurani, unyenyekevu, mtu wa hali ya kawaida, ukweli, kupa nyongo ulimwengu, tabia njema, fikra ya kuhifadhi imani na kueneza elimu ya dini na kuwatakiya heri waislamu.

Kupitia shirika la Dawat-e-Islami, ameleta mageuzi ya kimadani kwa mamilioni ya waislamu, hasa vijana wa kiislamu wa kike na wa kiume. Vijana wengi wametubia dhambi zao na wanafuata njia ya uongofu. Wale waliokuwa hawaswali, sio kuswali tu bali sasa wanaswalisha. Waliokuwa wakiwakosea adabu wazazi wao, sasa wanawatwii. Waliokuwa katika giza la ukafiri sasa wamebarikiwa na nuru ya uislamu. Waliokuwa na tamaa ya kuona ‘mapambo’ ya ulaya sasa wanahamu ya kuiona Al-Ka’abah

tukufu na kuzuru kuba la kijani (Msikiti Mtukufu wa Madina). Waliokuwa wameghilibiwa na ulimwengu, sasa wanafikiria zaidi maisha yao ya baada ya kufa. Waliokuwa wakipenda kusoma vitabu vichafu vya riwaya sasa wanasoma vitabu vya wanavyuoni wa Ahl-e-Sunnat **دَامَتْ نُورُهُمْ** na vitabu vingine vya kidini. Waliokuwa wakipenda safari za kustarehe, sasa wanasafiri na Madanī Qāfilāh pamoja na wapenzi wa Mtume **صَلَّى اللهُ تَعَالَى عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ** katika njia ya Allah **عَزَّوَجَلَّ**. Waliokuwa lengo lao la maisha ni kukusanya mali, sasa wameazimia: “Nitajaribu kusuluhisha nafsi yangu na watu wa ulimwengu mzima” **إِنْ شَاءَ اللهُ عَزَّوَجَلَّ**”

صَلُّوا عَلَى الْحَبِيبِ صَلَّى اللهُ تَعَالَى عَلَى مُحَمَّدٍ

Dawat-e- Islami katika Mataifa 176

Kwa rehema za Allah **عَزَّوَجَلَّ** na huruma za Mtume **صَلَّى اللهُ تَعَالَى عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ**, na baraka za maswahaba wa Mtume **صَلَّى اللهُ تَعَالَى عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ** na kufungamana na mawalii **رَحْمَةُ اللهِ تَعَالَى**, na msaada wa maulamaa na mashekhe na juhudi za Amīr-e-Ahl-e-Sunnat **دَامَتْ بَرَكَاتُهُمُ الْعَالِيَةَ** ujumbe wa Dawat-e-Islami umeenea Pakistan mwote na tulipokuwa tukiandika kitabu hiki, ulikuwa umeenea katika mataifa 176 ulimwenguni ikiwemo India, Bangladesh, nchi za Kiarabu, Sri Lanka, Uingereza, Australia, Korea na Afrika Kusini. Na bado juhudi zinaendelea kueneza ujumbe ufike mbali zaidi **الْحَمْدُ لِلَّهِ عَلَى إِحْسَانِهِ**.

اَلْحَمْدُ لِلّٰهِ عَزَّوَجَلَّ Kwa sasa (1433 H) Dawat-e-Islami inaitumikia dini katika nyanja zaidi ya 63. Ijtimai za kila wiki za kufundisha sunna zinafanyika katika sehemu nyingi ulimwenguni; Walinganizi wasio hisabu wanasafiri katika Madani Qafilah kufundisha sunna na kusuluhisha umma kwa jazba ya: “Nitajaribu kusuluhisha nafsi yangu na watu wa ulimwengu mzima” اِنْ شَاءَ اللّٰهُ عَزَّوَجَلَّ

صَلُّوْا عَلَيَّ الْحَبِيْبِ صَلَّى اللّٰهُ تَعَالٰى عَلٰى مُحَمَّدٍ

Ulinganizi kati ya Wasio Waislamu

Kwa juhudi zake na uhusiano mwema na watu, Shaykh-e-Tariqat Amīr-e-Ahl-e-Sunnat داعية بركاتها في العالمين aliwafunza ndugu waislamu na kutia ndani ya mioyo yao fikra ya kujisuluhisha pamoja na watu wote wa ulimwengu. Na kwa juhudi zao wenyewe ndugu waislamu hawa wameweza kueneza mwito huu na kuwalingania watu katika kufanya mema. Kwa mamilioni, wapotevu wamekuwa waislamu wa matendo na wanaswali kwa wakati wake na wanafuata sunnah na ambao hawakuwa waislamu wameanza kusilimu katika mataifa mbalimbali kutokana na juhudi za walinganizi wa Dawat-e-Islami.

Kafiri Asilimu

Enyi ndugu wapenzi waislamu! Madani Qafilah ya siku 92 kutoka Madani Markaz ya Dawat Islami, Faizan-e-Madinah, Bab ul Madinah Karachi Pakistan ilifika Colombo (Sri Lanka).

Walipokuwa tayari kuondoka kwenda wilaya ya Aero kwa siku 30, muislamu mmoja alimleta kafiri mmoja kwa amiri wa Qafilah.

Baada ya kumuelezea baadhi ya tabia njema za Mtukufu Mtume صَلَّى اللهُ تَعَالَى عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ, yule amiri wa Madani Qafilah alimshauri kuingia katika Uislamu. Yule kijana akamuuliza maswali na baada ya kujibiwa na kuridhika akasilimu اَلْحَمْدُ لِلّٰهِ عَزَّوَجَلَّ. (Faizān-e-Sunnat, Bāb: Ādāb-e-Ṭa'ām, Juz 1, uk. 261)

“Ya Allah عَزَّوَجَلَّ! Wape istiqama (msimamo) walioingia katika uislamu hivi karibuni na kwa baraka zao tupe nasi istiqama!”

آمِينَ بِجَاهِ النَّبِيِّ الْأَمِينِ صَلَّى اللهُ تَعَالَى عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ

صَلُّوا عَلَى الْحَبِيبِ صَلَّى اللهُ تَعَالَى عَلَى مُحَمَّدٍ

Madani Qafilah

Kwa kufuata nyayo za mawalii wa Kiislamu, Amīr-e-Ahl-e-Sunnat دَامَتْ بَرَكَاتُهُمُ الْعَالِيَةَ alikuwa akisafiri katika njia ya Allah عَزَّوَجَلَّ tangu Dawat-e-Islami ianzishwe, katika miji na vijiji vya mbali na sehemu za ndani ndani ima kwa basi au gari moshi ili kutoa bayana, mara nyingine zaidi ya bayana moja kwa siku. Alipokuwa akitembelea maeneo ndani ya Babul Madina (Karachi), alijichukulia chakula chake, ikiwemo chumvi na maji ili asije kusumbua watu.

Katika siku za mwanzo alikuwa akitembea usiku wa manane masafa ya karibu kilomita 5 au 6 baada ya kushukishwa na basi kwa kuwa hakuwa na nauli ya kukodisha teksi au tuktuk. Mbali na kuwalingania katika dini alikuwa pia akiwatembelea wagonjwa na waliofiwa ili awafariji kwa msiba wao na alipoondoka huwa wameathirika kiasi kikubwa na ziara yake. Juhudi hizi zimeendelea na kupanuka. Hii leo Madani Qafilah zisizohesabika za wapenzi wa Mtume ﷺ husafiri nchi hadi nchi, wilaya hadi wilaya, mji hadi mji kwa siku 3, 12, na 30 au miezi 12 au 26 wakieneza elimu ya dini, sunnah na mwito wa kufanya mema.

Nyuso Memetefu Zinasababisha Kusilimu

Katika mwaka 1425H (Januari 2005) Nigran wa Majlis-e-Shura ya Dawat-e-Islami na baadhi ya wanakamati wa Majlis-e-Berun-e-Mumalik (Baraza la nchi za ng'ambo) walikwenda na Madani Qafilah huko Afrika kusini ili kuangalia kipande cha ardhi kitakachojengewa Madani Markaz ya Dawat-e-Islami, wenyeji waliwakaribisha kwa mikono mikunjufu.

Mwenye ardhi hiyo, ambaye alikuwa ni mkristo, alipowaona wageni wake waliokuwa wamevaa vilemba vya kijani na nyuso memetefu zenye madevu, aliathirika sana. Akasongea mbele na akamwambia Nigran wa Shura: “Tafadhali nisilimishe niwe muislamu.” Hapo hapo alipigishwa shahada na akasilimu. Ndugu wote waliokuwa pale walifurahishwa sana na tukio hilo

na wakataja jina la Mwenyezimungu, “Allah! Allah!” Sauti zao zikatetemesha anga.

Tanbihi: ili kujuwa mengi kuhusu baraka za Madani Qafilah na mafunzo mengi kuhusu Uislamu soma kitabu ‘*Faizān-e-Sunnat*’ (Juzuu 1) na ‘*Dawat-e-Islami kī Madanī Bahārāin*’ vinavyopatikana katika maduka ya Maktaba-tul-Madīnah.

صَلُّوا عَلَى الْحَبِيبِ صَلَّى اللَّهُ تَعَالَى عَلَى مُحَمَّدٍ

Vituo vya Masomo vya Madani

Ili kueneza vizuri mwito wa kufanya mema, vituo vya masomo vya Madani vimefunguliwa katika miji mingi ulimwenguni kwa kufuata rai ya Amīr-e-Ahl-e-Sunnat رَاعَتْ بَرَكَاتِهِمُ الْعَالِيَةَ.

Katika vituo hivi vya Madani waislamu kutoka kila pembe huja kujifunza sunna na kukaa pamoja na wapenzi wa Mtume صَلَّى اللهُ تَعَالَى عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ kisha wanaeneza mwito wa uongofu. Kuna wasaidizi ambao husaidia hata wale ambao wana wakati mchache (kutoa kwa ajili ya Allah عَزَّوَجَلَّ) angalau wapate faida fulani ya elimu ya dini.

Kujenga Misikiti

Ni matarajio ya Amīr-e-Ahl-e-Sunnat رَاعَتْ بَرَكَاتِهِمُ الْعَالِيَةَ kwamba misikiti yote iimarike kama ilivyokuwa zamani. Pamoja na kuimarisha misikiti, mingine iendelee kujengwa. Ili kutimiza

lengo hili, Majlis-e-Khuddam-ul-Masajid (Baraza la Wahadimu wa Misikiti) limeundwa. Kila kukicha kuna ujenzi wa misikiti unaoendelea.

الْحَمْدُ لِلَّهِ عَزَّوَجَلَّ Vile vile Madanī Marākiz yaani Faizan-e-Madinah yameshajengwa katika nchi kadhaa na bado yanaendelea kujengwa kutokana na ruhusa ya Majlis-e-Shura.

Gharama za ujenzi wa Madanī Marākiz, Jāmi'a-tul-Madīnah, Madāris-ul-Madīnah na shughuli zingine za Dawat-e-Islami zinadhaminiwa na michango ya waislamu. Si kila mtu anakubaliwa kukusanya michango bali ni sharti kupatikana idhini ya Markazi Majlis-e-Shura.

Maimamu Wa Misikiti

Kuna kamati za misikiti nyingi ambazo haziwezi kugharamia usimamizi wa maimamu, waadhini na wafanyikazi wa misikiti. Dawat-e-Islami hujitolea kuwasaidia watu hawa kwa kuwapa mishahara.

Viziwi, Mabubu na Vipofu

Kwa rehema za Allah عَزَّوَجَلَّ na juhudi za Amīr-e-Ahl-e-Sunnat دَامَتْ بَرَكَاتُهُمُ الْعَالِيَةَ ndugu zetu waislamu mahsusi (walemavu, k.m mabubu, viziwi na vipofu) wanapata mafunzo ya dini ya Kiislamu. Hawa ni watu wanaodharauliwa katika jamii. Wengine wao huwa hawana hata elimu ya chini kabisa kwa sababu ya kutengwa.

أَلْحَمْدُ لِلَّهِ عَزَّوَجَلَّ kwa natija ya kufuata mwenendo wa Amīr-e-Ahl-e-Sunnat دَامَتْ بَرَكَاتُهُمُ الْعَالِيَةَ na kwa juhudi za Majlis ya waislamu mahsusi leo katika miji mingi ya Pakistan kwenye ijtimai ya kila wiki na wakati wa siku za itikaf katika Ramadhani waislamu mahsusi wanakusanyika mahali pamoja ambapo kasida, bayana, dhikri na du'a hutafsiriwa kwa lugha ya ishara.

Aidha, kuna kozi ya siku 30 ya Qufl-e-Madinah inayowafundisha walinganizi kuelewa lugha ya ishara, ili waweze kueneza ujumbe kwa ndugu zetu walemavu. Madani Qafilah za walemavu pia nazo husafiri.

Kafiri Asilimu

Katika mwaka 2007 Madani Qafilah moja ya vipofu walipanda basi kuelekea msikiti mmoja Karachi. Waliandamana na waislamu ambao si walemavu. Amiri wa Qabila hii akaanzisha mazungumzo na mtu aliyekaa karibu naye.

Yule mtu akasema, “Mimi si muislamu, nimeusoma Uislamu na nimependezewa nao lakini pingamizi ya kuingia katika Uislamu ni tabia mbaya ya baadhi ya waislamu. Lakini nimewaona nyinyi namna mulivyovalia nadhifu, nguo nyeupe na mumetoa salamu mulipoingia ndani ya basi. Cha kushangaza zaidi ni vipofu mulioandamana nao pia wamevalia kanzu nyeupe na vilemba vya kijani na wameweka ndevu.”

Baada ya kumsikiliza, yule Amiri wa Qafilah alimueleza kwa muhtasari kuhusu Majlis ya Waislamu Mahsusi kisha

akamuelezea kuhusu huduma kubwa za kidini za Amīr-e-Aḥl-e-Sunnat **دَامَتْ بَرَكَاتُهُمُ الْعَالِيَةَ**. Pia alimueleza kuhusu Dawat-e-Islami. Halafu akafafanua, “Hao ndugu vipofu unaowaona wanakwenda kuwaregesha kwenye njia ya haki wale waislamu waovu wanaokufanya wewe kuogopa kuingia kwenye Uislamu.” Baada ya kusikiliza maneno haya aliathirika na alipiga shahada na kusilimu.

Tanbihi: Ili kusoma zaidi kuhusu matukio ya vipofu, mabubu na viziwi soma kitabu ‘*Goonga Muballigh*’ kilichochapishwa na Maktaba-tul-Madinah.

Ulinganizi Gerezani

Kwa kawaida wale waliokosa elimu ya Qur’an na Sunnah hudanganywa na nafsi zao na shetani ndiyo wakaingilia kufanya makosa makubwa kama vile kuua, ugaidi, wizi, uzinifu, kuuza madawa ya kulevya, kamari na mwishowe huishilia gerezani.

اَلْحَمْدُ لِلّٰهِ عَزَّوَجَلَّ Dawat-e-Islami, chini ya Majlis Faizan-e-Qur’an inafundisha wafungwa gerezani. Wahalifu wengi huathirika na kazi za Dawat-e-Islami, hutubia na wanapotoka gerezani huandamana na Madani Qafilah na wanaishi maisha kwa mujibu wa sunnah.

Wengi ya waliokuwa wakiwamiminia watu marisasi sasa wanawarushia lulu za sunnah. Kutokana na juhudi za walinganizi wa Dawat-e-Islami hata wafungwa makafiri wanasilimu.

Habusu Arekebishika

Shaykh-e-Tariqat, Amir-e-Ahl-e-Sunnat, ‘Allāmah Maulānā Abu Bilal Muhammad Ilyas Attar Qadiri Razavi Ziyāe دَامَتْ بَرَكَاتُهُمُ الْعَالِيَةَ amesema kwamba shughuli za Dawat-e-Islami zimendelea sana gerezani. أَلْحَمْدُ لِلَّهِ عَزَّوَجَلَّ Mbali na kusikiliza bayana pia wafungwa wanafundishwa kusoma Qur’ani na sheria za dini ya Kiislamu. Wale ambao walikuwa wagumu kubadilika kwa kutumia viboko wameweza kubadilishwa na mazingira ya Dawat-e-Islami.

Tulipata barua kutoka kwa dada yetu muislamu kutoka wilaya ya Kasur Dak-khana Khuddian (mji wa sufi mkubwa anayelitwa Baba Bulleh Shah رَحْمَةُ اللهِ تَعَالَى عَلَيْهِ) akisema, “Ni miaka minane sasa tangu nifiwe na mume wangu na nina mtoto mmoja tu wa kiume. Lakini mtoto huyu kwa sababu ya marafiki wabaya alikuwa mtundu sana. Hasikii na kila mara hujiingiza katika visa vya uhalifu na pia huuza madawa ya kulevya. Aliwahi kushikwa mara kadhaa na polisi na mimi kila mara hufanya juhudi kumtoa. Alikuwa na kesi nyingi na moja wapo ilisababisha yeye kufungwa gerezani. Baada ya kupita karibu miezi minane alitolewa jela kwa dhamana. Aliporudi nyumbani mimi nikashtuka. Sikuweza kuamini vile nilivyomuona, mtoto huyu huyu aliyekuwa muovu akinipiga, akinitukana na mwenye tabia mbaya leo ameniangukia miguuni akiniomba msamaha huku akilia.

Mara adhana ya swala ya Magharibi ikaadhiniwa, mtoto huyu akaenda zake msikitini. Sasa ni mtulivu, mpole na tena uso wake

unang'ara. Kijana huyu aliyekuwa akitukana kila mara sasa anatamka *إِنْ شَاءَ اللَّهُ، مَا شَاءَ اللَّهُ، الْحَمْدُ لِلَّهِ، سُبْحَانَ اللَّهِ* na kumswalia Mtume *صَلَّى اللهُ تَعَالَى عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ* kila wakati. Baada ya kuswali swala ya isha alirudi nyumbani na akalala mapema, nami nikapata kujipumzisha. Usiku wa manane niliamka nisimkute kitandani nikadhani tayari ameshatoroka kwenda kuiba lakini nikashangaa nilipomkuta yuko kipembeni anaswali tahajjudi kwa unyenyekevu. Alipomaliza swala yake akaleta du'a hii:

Niokowe na dhambi, ya Ilahi

Niokowe na tabia mbaya, ya Ilahi

Zifute dhambi zangu, ya Ilahi

Nifanye mimi mtu mwema, ya Ilahi

Kwa jaha ya Manabii wote, ya Ilahi

Nisamehe kila dhambi yangu, ya Ilahi

Nilipomuona mtoto wangu analia nami nikalia na kumkumbatia. Sote tulilia kwa muda. Baada ya kunyamaza nikamuuliza sababu ya mabadiliko haya akaniambia, “Ni mazingira mazuri ya Dawat-e-Islami niliyoyapata huko jela. Walinganizi wao walifundisha watu kutawadha, kuswali, kufanya sunnah, du'a na kusoma Qur'an sawasawa. Nilitubia kutokana na juhudi za wapenzi wa Mtume *صَلَّى اللهُ تَعَالَى عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ*.”

Nilifurahi sana kwa aliyonieleza. Nawashukuru walinganizi wa Dawat-e-Islami kwa kumbadilisha mwanangu aliyekuwa muovu mkubwa. Dawat-e-Islami imenifanyia ihsani kubwa mjane kama

mimi, tena mama maskini. Ewe Allah **عَزَّوَجَلَّ** kina mama wote ambao wana huzuni kwa kuwa wana wao wako jela, wana hawa wabarikiwe na mazingira ya Dawat-e-Islami ili waepukane na uhalifu na waanze maisha mapya ya sunnah za Mtume mtukufu **صَلَّى اللهُ تَعَالَى عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ**.”

Tanbihi: ili kusoma visa zaidi kama hivi soma kitabu ‘Services of Dawat-e-Islami in Jails’ kutoka tawi lolote la Maktaba-tul-Madīna.

صَلُّوا عَلَى الْحَبِيبِ **صَلَّى اللهُ تَعَالَى عَلَى مُحَمَّدٍ**

Itikaf ya Pamoja

Miaka miwili au mitatu kabla ya kuasisiwa kwa Dawat-e-Islami, Amīr-e-Ahl-e-Sunnat **دَامَتْ بَرَكَاتُهُمُ الْعَالِيَةِ** alifanya itikaf peke yake katika Msikiti Nur ulioko Soko la Karatasi, eneo la Mithadar Bab-ul-Madinah (Karachi) ambapo yeye alikuwa ni Imam. Mwaka uliofuata, kutokana na juhudi zake, ndugu wawili walimuunga katika itikaf. Kwa sababu ya juhudi zake na tabia njema aliyonayo, idadi ya wenye kufanya itikaf iliongezeka kila mwaka na kufikia 28. Habari zilipoenea kuhusu itikaaf ya watu 28 tena vijana, watu walishangaa na wakaja kuwazuru.

اَلْحَمْدُ لِلّٰهِ عَزَّوَجَلَّ Mwaka huo huo, Dawat-e-Islami ikaanzishwa na katika Madani Markaz ya kwanza - Msikiti wa Gulzar-e-Habib (Gulistan-e-Okarvi, Bab-ul-Madinah Karachi) ilifanyika itikaf ya watu 60 ya pamoja. Walibahatika kuwa pamoja na Amīr-e-

Ahl-e-Sunnat **دَامَتْ بَرَكَاتُهُمُ الْعَالِيَةَ**. Mtindo huo wa kufanya itikaf kwa pamoja unaendelea sana sio tu katika Pakistan bali hata na nje yake pia katika mwezi Mtukufu wa Ramadhan, kwa siku 30 au siku kumi za mwisho. Maelfu ya ndugu waislam huhudhuria itikaf hizi na kujifunza elimu ya dini na sunnah, mbali na kufanya ibada zingine. Pia, wana itikaf wengi husafiri katika Madani Qafilah katika usiku wa kuamkia Iddul Fitr. Wengi wa akina dada waislamu pia hufanya itikaf majumbani mwao ambapo wao pia hujifunza mengi kuhusu Uislamu.

Tanbihi: ili kusoma zaidi kuhusu itikaf ya pamoja soma sura 'Blessings of Ramadhan' katika *Faizān-e-Sunnat* (Juz. 1) na ununue kijitabu 'Dawat-e-Islami kī Bahārāin' kutoka tawi lolote la Maktaba-tul-Madīnah.

صَلُّوا عَلَى الْحَبِيبِ صَلَّى اللَّهُ تَعَالَى عَلَى مُحَمَّدٍ

Ijtimai kubwa baada ya Hajj

Mbali na maelfu ya ijtimai zinazofanyika kila wiki katika nchi tofauti duniani, pia kuna ijtimai ya mkoa na ijtimai ya kimataifa. Baada ya ijtimai hizi, maelfu ya wapenzi wa Mtume **صَلَّى اللَّهُ تَعَالَى عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ** waliobahatika husafiri na Madani Qafilah. Ijtimai ya kimataifa ya siku tatu hufanyika katika mji wa Madina-tul-Awliya Multaan Shareef katika uwanja wa Sehra-e-Madina. Katika ijtimai hii watu kutoka sehemu mbali mbali za ulimwengu huja kushiriki. Bila shaka huu ni mkusanyiko

mkubwa wa waislamu baada ya hajj! ('Sehra-e-Madina' iliyoko Madina-tul-Awliya Multaan Shareef na iliyoko Babul Madina Karachi ni viwanja vikubwa mno na ni milki ya Dawat-e-Islami.) Kuna Majalis tofauti zinazoshughulikia maandalizi ya ijtimai.

Mabadiliko ya KiMadani kwa Kina Dada wa Kiislamu

Mamilioni ya akina dada wa Kiislamu wameukubali ujumbe wa KiMadani wa Dawat-e-Islami. Akina dada wengi waliiolewa katika jamii chafu wametubia dhambi zao na kuwa vipenzi vya mama wa wauminina رَضِيَ اللهُ تَعَالَى عَنْهُنَّ (wake za Mtume صَلَّى اللهُ تَعَالَى عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) na mwana wa Mtume صَلَّى اللهُ تَعَالَى عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ, Nana Fatimah رَضِيَ اللهُ تَعَالَى عَنْهَا. Waliokuwa wakitembelea maduka makubwa bila staha, majumba ya anasa, vilabu na sinema sasa wameifanya Madani Burqa (vazi kubwa kama buibui linalofunika kichwa mpaka vidole vya miguuni) kuwa ndilo vazi lao, wakifuata nyayo za wanawake wenye heshima ya hali ya juu waliosimama Karbala. Idadi ya ijtimai za kila wiki za akina dada zinafanywa katika sehemu nyingi huku wakichunga hijabu ya Kiislamu.

Vyuo kadhaa vya wasichana vimefunguliwa ambapo wanahifadhi Qur'ani na wanajifunza kusoma Qur'ani kwa sawasawa bila ya malipo yoyote. Isitoshe, Jamiat-ul-Madina ya wasichana zimefunguliwa ili wajifunze na wawe wanavyuoni wa kike. Idadi ya akina dada waliohifadhi Qur'ani na

wanavyuoni wa kike inaongezeka katika Dawat-e-Islami. Kwa ufupi, dada waislamu si dhaifu wakilinganishwa na akina kaka wa Kiislamu.

Mifano kidogo ya Shughuli za Mwezi za akina Dada

Mfano wa shughuli zilizofanywa na akina dada wa Kiislamu katika Pakistan katika mwezi wa Mfungo Sita 1433H (Februari 2012). Orodha hii tulipewa na Baraza Kuu la Akina Dada wa Kiislamu wa Pakistan

- i. Darsa 52157 zilifanywa majumbani.
- ii. Inakisiwa kuwa Madāris-ul-Madīnah Baleghat kwa watu wazima wanawake ambazo zinazofanywa kila siku Pakistan zimefikia idadi ya 2645, ambapo kina dada 30136 walishiriki, kujifunza kusoma Qur'ani na sunnah pamoja na kuhifadhi du'a mbalimbali.
- iii. Takriban ijtimai 4521 za kila wiki zilifanywa ambapo akina dada 115175 walishiriki.
- iv. Vipindi vya mafunzo karibu 6375 vya kila wiki vilifanywa.

صَلَّى اللّٰهُ تَعَالَى عَلٰى مُحَمَّدٍ

صَلُّوْا عَلٰى الْحَبِيْبِ

Tazama namna Mazingira ya KiMadani yanavyombadilisha mui kuwa mwema!

Huu ni mukhtasari wa kisa alichotuelezea dada yetu kutoka Bāb-ul-Madīnah Karachi. Alisema, “Nilihifadhi Qur’ani nikiwa mdogo kutokana na msukumo wa wazazi wangu. Walakini baada ya kuhifadhi si kushughulika tena kuisoma. Ingawa nilibahatika kuhifadhi Qur’an, mara nyingine nilikuwa si swali swala zote bali nilishika nyimbo na kuangalia televisheni sana. Hata siku zingine nilikuwa nikikesha kusikiliza muziki. Nilikuwa mraibu wa kutazama filamu. Pia nilikuwa shabiki wa muimbaji mmoja hadi nikikosa kukiangalia kipindi chake kimoja huwa na tokwa na machozi na mara nyingine huacha kula pia. Nilimpenda mno hata wenzangu wakaniambia kuwa nitamtaja muimbaji huyo hata wakati wa sakaratul mauti. Kweli nilikuwa katika dimbwi la uchafu!

Mmoja wa makhale (shangazi) zangu alikuwa heshi kunialika twende kwenye ijtimai za kila wiki ili nipate uongofu lakini kila mara nilitoa udhuru. Hakuacha kunivuta mpaka siku moja nilimfuata katika ijtimai kusikiliza bayana, Žikr ya Allah عَزَّوَجَلَّ na du'a zilizozigusa moyo. Pia Halqah Nigran (msimamizi wa eneo wa kike) alinipa moyo, alinibembeleza na alikuwa akinifuata nyumbani ili tuende kwenye ijtimai.

Dada huyu aliniusia nizekatae filamu, nyimbo na dhambi zinginezo. Nilisikiza kaseti za Maktaba-tul-Madinah kuhusu khutba za sunnah hadi zikaniathiri kumcha Allah عَزَّوَجَلَّ zaidi.

Pia, vitabu vilivyochapishwa na Maktaba-tul-Madinah vilinipa moyo wa kutaka kuwasaidia wenzangu katika kazi ya kulingania watu katika kufanya mema. Kila nililoambiwa nifanye na Zimmadar (msimamizi) wangu nililifanya kwa dhati.

اَلْحَمْدُ لِلّٰهِ عَزَّوَجَلَّ Niliendelea kutekeleza wajibu wangu kwa Dawat-e-Islami na sasa nimepewa jukumu la kuwa Zimmadār (msimamizi) wa ‘Alāqah̄ Mushāwarat.

Nilikuwa nimesikia kuwa Muftī wa Dawat-e-Islami Hāfiẓ Muhammad Fārūq ‘Aṭṭārī Al-Madani عَلَيْهِ رَحْمَةُ اللّٰهِ الْعَلِيِّ alikuwa akisoma manzil (juzuu nne) moja kati ya saba za Qur’an wakati alipokuwa mwanafunzi. Nami nimeanza kusoma manzil moja kila siku. Ewe Allah عَزَّوَجَلَّ! nipe msimamo!

صَلُّوْا عَلٰى الْحَبِيْبِ صَلَّى اللّٰهُ تَعَالٰى عَلٰى مُحَمَّدٍ

Madani In’āmāt

Shaykh-e-Ṭarīqat, Amīr-e-Aḥl-e-Sunnat رَاضِيَةٌ بَرَكَاتُهُمُ الْعَالِيَةِ ametengeneza mkusanyo wa tafsili wa Shari’ah̄ na Ṭarīqah̄ uitwao 'Madani In’āmāt’ katika mbinu ya hojaji yenye lengo la kukurahisishia kutenda mema na kuepuka na dhambi katika zama hizi za fitna. Kuna maswali 72 ya Madani In’āmāt kwa ndugu waislamu wa kiume, 63 kwa akina dada wa kiislamu, 92 kwa wanafunzi wa kiume wa kiislamu, 83 kwa wanafunzi wa kike wa kiislamu, 40 kwa watoto, na 27 kwa ndugu walemavu (vipofu, mabubu na viziwi).

Wengi wa ndugu wa kiislamu, kina dada, na wanafunzi wanajaza kijitabu cha Madani In'āmāt kila siku usiku kabla ya kulala. Kwa rehema za Allah ﷺ kwa kufuata Madani In'āmāt viziwi ambavyo mtu hupata katika kufuata njia ya uongofu na kuepokana na madhambi huondoka. Vile vile kwa baraka za Madani In'āmāt, mtu anakuwa mwenya kufuata sunna, kuchukua madhambi na mwenye kuwa na fikra ya kulinda imani.

Ili kuwa muislamu wa kikweli kweli, kila mmoja apate hicho kijitabu cha Madani In'āmāt kutoka kwenye tawi lolote la Maktaba-tul-Madīnah akijaze kila siku anapofanya fikr-e-Madīnah. Pia mtu afanye mazoea ya kumkabidhi Zimmadār wa Madani In'āmāt wa eneo lake katika siku 10 za mwanzo wa mwezi wa kiislamu.

صَلُّوا عَلَى الْحَبِيبِ صَلَّى اللَّهُ تَعَالَى عَلَى مُحَمَّدٍ

Bishara njema kwa wanaofuata Madani In'āmāt

Ndugu wapenzi waislamu! Wamebahatikaje wenye kufuata Madani In'āmāt! Soma kisa kifuatacho cha Madani na ufurahike. Ndugu yetu muislamu kutoka Hyderabad (Bāb-ul-Islam, Sindh) alitupa kauli ifuatayo na akaapa: “Siku moja katika mwezi wa Rajab nilibahatika kumuota Mtume mtukufu صَلَّى اللَّهُ تَعَالَى عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ. Mtume صَلَّى اللَّهُ تَعَالَى عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ akaniambia, “Mwenye kufanya fikr-e-Madina kila siku kwa kutumia Madani In'āmāt basi Allah ﷺ atamsamehe.” (*Faizān-e-Sunnat, Bāb: Faizān-e-Ramadan, Juz 1, uk. 1135*)

Madani Muḏākaraḥ

Kwa hakika kuwa pamoja na Amīr-e-Aḥl-e-Sunnat داعية بركة الله العالیه ni bahati kubwa. Ndugu wengi waislamu huchukua fursa hii kukutana naye katika Madani Muḏākaraḥ zinazofanyika sehemu tofauti na kuuliza maswali kuhusu imani na amali, shari'ah na tariqah, historia na sera, sayansi na tiba, maadili na ikhlas, habari kuhusu Uislamu na Uchumi, maswala ya kijamii na mambo kuhusu Dawat-e-Islami na mada zinginezo.

Shaykh-e-Tariqat, Amīr-e-Aḥl-e-Sunnat داعية بركة الله العالیه huwajibu kwa ufasaha na hekima kwa njia iliojaa mapenzi ya Mtume صلى الله تعالى عليه وآله وسلم. Pia kila anapojibu swali huwahimiza watu kumsalia Mtume Mtukufu صلى الله تعالى عليه وآله وسلم.

Tiba ya Kiroho na Istikharah

Moja kati ya mabaraza ya Dawat Islami lijulikanalo kama 'Majlis Maktūbāt na Ta'wizāt-e-Atṭāriyyāh' linajishughulisha kuwapa waislamu wagonjwa tiba za kiroho bila malipo. Huwapa Ta'wizāt (hirizi) zilizokubaliwa na Shaykh-e-Tariqat, Amīr-e-Aḥl-e-Sunnat, 'Allāmah Maulānā Muhammad Ilyas Attar Qadiri داعية بركة الله العالیه. Pia istikharah hufanywa kuwafaidi waislamu wengi kila siku.

Bila ya kutia chumvi mamilioni ya Ta'wizāt na baruwa za faraja hutumwa kila siku kwa waislamu. Aidha, kulingana na kukisia (wakati tulipoandika kitabu hiki) takriban Ta'wizāt na

dua ambazo hutolewa kwa wahitaji kila mwezi ni 225000 na kila mwaka ni 2600000. Kila mwezi karibu baruwa 20000 hadi 25000 hujibiwa (pamoja na zile zinazojibiwa kwa mtandao).

Wale wanaotaka Ta'wizāt wahudhuriye ijtimai za kila wiki zinazofanyika katika miji yao na watapata meza ambamo munapatikana Ta'wizāt-e-'Aṭṭāriyyāh. Kuna manufaa mengi yamepatikana kutokana na Ta'wizāt-e-'Aṭṭāriyyāh.

Uvimbe wa Ubongo

Ndugu yetu muislamu kutoka Sak-khar (Bab ul Islam, Sindh) ametupa kisa hiki na kuapa kwamba: “Mtu mmoja kutoka eneo letu alikuwa na uvimbe wa ubongo na alikuwa amefanyiwa upasuaji mara mbili na hakupata afueni. Alikuwa katika hali ya kusikitisha. Hata madaktari walikuwa wamekata tamaa ya mgonjwa kupona. Mtu mmoja aliwashauri nduguze waende wakachukue Ta'wizāt-e-'Aṭṭāriyyāh lakini hawakulitilia maanani jambo hili.

Siku moja, nduguye mdogo wa kiume, akiwa amefadhaika na kuhuzunika, alikuja kwenye meza ya Ta'wizāt-e-'Aṭṭāriyyāh na akasema huku akilia, “Ndugu yangu mkubwa yuko katika hali mahututi na nadhani leo ndiyo siku yake ya mwisho. Hamtambui yeyote na hata pumzi hawezi kuvuta sawasawa; tafadhali nipeni Ta'wizāt za kumponya.” Ndugu wa Majlis alimfariji na kumwambia, “Usihuzunike Allah عَزَّوَجَلَّ ndiye mponyaji. Chukua hizi Ta'wizāt na kwa baraka yazo atapona kama walivyopona

wagonjwa wengi ambao madaktari walikuwa wamewakatia tamaa.” Siku ya pili, nduguye akiwa na uso wa bashasha, alikuja katika meza ya Ta’wizāt-e-‘Atṭāriyyāh na akasema, “Nilipofika nyumbani nilimfunga ndugu yangu ambaye alikuwa anaonekana kama yuko katika pumzi zake za mwisho Ta’wiz kichwani na baada ya muda mfupi akafungua macho akawaacha jamaa wote vinywa wazi. Halafu akawaashiria jamaa zake wamkalishe. Na **صَلَّى الْحَمْدُ لِلَّهِ عَزَّ وَجَلَّ** akaanza kula.”

Baada ya siku mbili, yule mgonjwa alikuja kibandani mwenyewe kwa miguu yake ili akutane na wasimamizi wa Majlis-e-Ta’wizāt-e-‘Atṭāriyyāh ili awaarifu kuwa hali yake imeimarika kwa asilimia 75.

صَلُّوا عَلَى الْحَبِيبِ صَلَّى اللَّهُ تَعَالَى عَلَى مُحَمَّدٍ

Tanbihi: Ili kusoma zaidi kuhusu tiba ya kiroho, pata vijitabu hivi vilivyochapishwa na Maktaba-tul-Madīnah: ‘Khaufnāk Balā’, ‘Purisar Kuttā’, ‘Singaun Walī Dulḥan’ and ‘Khush Naṣīb Marīd.’

Kuwafunza Mahujjaji

Chini ya usimamizi wa Majlis ya Hajj na Umra, katika msimu wa Hajj, walinganizi wa Dawat-e-Islami huwafunza mahujjaji katika kambi za hajj. Vitabu vya miongozo ya hajj kama vile ‘*Rafīq-ul-Haramayn*’ hugawanywa bure kwa mahujjaji ili

kuwaongoza kufanya ibada ya hajj na kuuzuru mji wa Madina Munawarrah.

Taasisi za Ilimu

Shaykh-e-Ṭarīqat, Amīr-e-Aḥl-e-Sunnat داعية بركاتهم العالیه amesema, “Wanafunzi ni hazina kubwa ya nchi na ndiyo viongozi wa kesho wa taifa. Ikiwa watafunzwa shariah na sunnah basi ucha Mungu na kumpenda Mtume صَلَّى اللهُ تَعَالَى عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ utasambaa katika jamii nzima.” Ili kuwaelimisha walimu na wanafunzi juu ya sunnah za Mtume صَلَّى اللهُ تَعَالَى عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ shughuli za Madani zinaendelezwa katika taasisi za elimu kama vile madrasa, shule na vyuo vikuu. Wanafunzi bila hisabu wanahudhuria ijtimai za kila wiki na husafiri na Madani Qafilah.

Wanafunzi kadhaa waliokuwa hawafanyi ibada sasa wana swali na wanafuata sunna. Pia kuna kozi ya ‘Faizan-e-Qur’an na Hadith’ inayofanyika wakati wa likizo ili kuwafunza wanafunzi masomo ya kidini.

Jamiatul Madina

Tawi la kwanza la Jāmi’a-tul-Madīnaḥ lilianzishwa chini ya usimamizi wa Dawat-e-Islami mnamo mwaka wa 1995 katika gorofa ya pili katika Madrasa-tul-Madīnaḥ, Godrah colony, New Karachi, Bāb-ul-Madīnaḥ Karachi. Baada ya muda kupita, matawi mengine yakafunguliwa. Wakati huu ninapo andika haya, (yaani tarehe 30 Rabi’-un-Nūr 1433 A.H.) Jāmi’a-tul-Madīnaḥ 176

zimeanzishwa, ambapo takriban ndugu wa kiume waislamu 7000 wanafundishwa kuwa wanavyuoni (kuna huduma ya malazi na chakula inapohitajika). Vile vile kinadada waislamu karibu 3500 wanafundishwa kuwa wanavyuoni. Huduma zote hizi hutolewa bila malipo.

Wanafunzi wa Dawat-e-Islami wamepata ufanisi mkubwa katika mitihani inayotolewa na Tanzīm-ul-Madāris (Baraza Kuu la Mtihani La Madaris ya Ahl-e-Sunnat) Pakistan. Kila mwaka wanafunzi wa Jāmi'a-tul-Madīnah ima huchukua nafasi ya kwanza au ya pili au ya tatu au zote kwa pamoja. Mahafali hupewa cheo cha 'Madani' baada ya kukamilisha masomo yao.

Madrassa-tul-Madīnah

Madrassa-tul-Madīnah zimeanzishwa ili kutoa mafunzo ya kusoma na kuhifadhi Qur'an. Kufikia wakati wa kuandika kitabu hiki takriban Madāris-ul-Madīnah 1108 (kwa wavulana na wasichana) zinatoa mafunzo Pakistan. Takriban wasichana na wavulana 72000 wanafunzwa kusoma na kuhifadhi Qur'an bila malipo.

Madrassa-tul-Madīnah (kwa watu wazima)

اَلْحَمْدُ لِلّٰهِ عَزَّوَجَلَّ! Chini ya usimamizi wa Dawat-e-Islami (Shirika la Kimataifa la Kueneza Mafundisho ya Quran na Sunna lisilojihusisha na siasa), Madāris-ul-Madīnah (kwa watu wazima) yanatoa mafunzo ya kusoma Qur'an kisawasawa pamoja na dua,

kusali na sunna mbalimbali katika misikiti mbalimbali bila (wanafunzi) kutozwa malipo.

Kliniki

Kliniki zimefunguliwa ili kutoa matibabu kwa wafanyikazi na wanafunzi wagonjwa. Ikibidi, wagonjwa hulazwa au kuhamishwa katika mahospitali makubwa kwa matibabu. Katika Madani Markaz ya kimataifa Faizān-e-Madīnah Bāb-ul-Madīnah Karachi, kuna hospitali ndogo yenye vitanda 11 ambayo inatoa huduma ya matibabu ya kuridhisha.

Takhaṣṣuṣ-fil-Fiqh

Dawat-e-Islami pia ina andaa kozi ya mafunzo inayofanyika baada ya kumaliza Dars-e-Nizāmī inayoitwa Takhaṣṣuṣ-fil-Fiqh (utaalamu katika somo la Fiqhi) inayofanyika katika Jāmi'a-tul-Madīnah chini ya usimamizi wa wanavyuoni walioelimika. Kozi hii ni miaka miwili na ndugu wengi wa Dars-e-Nizāmī waliohitimu huwa wamesoma sayansi ya Fatwā. Kuna mtihani wa kiingilio ambao hufanyika ili kuchagua watakaojiunga na kozi. Wanafunzi hulipwa malipo kidogo ili wasipate matatizo ya kifedha katika masomo. Kwa sasa kozi hii inafanyika Jāmi'a-tul-Madīnah Faizān-e-Madīnah Bāb-ul-Madīnah Karachi peke yake.

Mbali na kupata mafunzo, wanafunzi wanatakiwa kupitia *Fatāwā Razaviyyah* (juzuu zote 30) na *Bahār-e-Sharī'at* (sehemu 20) wao wenyewe. Kando na hayo, ni muhimu kwa wanafunzi

kutwalii mkusanyiko mkubwa wa Fatāwā za mamufti wa Aĥl-e-Sunnat uliochapishwa kwa lugha ya ki Urdu. Baada ya hapo shahada ya kwanza ya Mutakhaṣṣiṣ-fil-Fiqĥ hutawazwa kwa yule anayeandika Fatāwā 1200 chini ya usimamizi wa mamufti. Yule anayeandika Fatāwā 1400 hupandishwa daraja ya kuwa naibu wa Mufti na mtu akiandika Fatāwā 1400 zaidi, kutokana na idhini ya Majlis ya Iftā ya Dawat-e-Islami, muhusika hupewa cheo cha Mufti na Muṣaddiq (yaani, yule aliyepewa mamlaka ya kuidhinisha Fatāwā). Pia hutolewa kozi ya mwaka mmoja ya Takhaṣṣuṣ-fil-Funūn na Tawqīt (utaalamu katika masomo mengine na somo kuhusu nyakati za swala).

Majlis Taḥqīqāt-e-Shar’iyyaĥ

Majlis-e-Taḥqīqāt-e-Shar’iyyaĥ ilianzishwa ili kutatua mambo mapya wanayokumbana nayo waislamu. Majlis hii ina mamufti na wanavyuoni wa Madanī wa Dawat-e-Islami.

Dār-ul-Iftā Aĥl-e-Sunnat

Dār-ul-Iftā Aĥl-e-Sunnat kadhaa zimeanzishwa katika sehemu mbalimbali ambapo wanavyuoni na mamufti wa Dawat-e-Islami wanashughulika kutoa muongozo kwa waislamu kuhusu Shariah. Wakati wa kuandika maelezo haya zaidi ya Fatāwā 45000 (pamoja na zinazotumwa kupitia intaneti) zinatolewa na matawi 10 ya Dār-ul-Iftā Aĥl-e-Sunnat yalioko katika miji mbalimbali ya Pakistan. Fatāwā nyingi hutolewa kwa kupitia machapisho.

Vile vile ndugu wengi waislamu hupata suluhisho la matatizo yao kulingana na Shari'ah kupitia kwa simu au kwa kumtembelea Dār-ul-Iftā wao wenyewe binafsi. **اَلْحَمْدُ لِلّٰهِ عَزَّوَجَلَّ**! Twatarajia maendeleo zaidi siku za usoni.

Mtandao

Ujumbe wa uislamu unasambazwa ulimwengu mzima kwa mtandao kupitia tovuti www.dawateislami.net na tovuti zingine za idara za Dawat-e-Islami.

Dār-ul-Iftā Ahl-e-Sunnat katika Mtandao

Huduma ya mtandao ya Dār-ul-Iftā Ahl-e-Sunnat inapatikana katika tovuti ya Dawat-e-Islami (www.dawateislami.net) ambapo maswali mbalimbali yanayoulizwa na waislamu yanajibiwa. Upinzani unaoletwa na makafiri dhidi ya uislamu hujibiwa na wao hulinganiwa kusilimu.

Maktaba-tul-Madīnah

Vitabu vingi mno vya A'la Ḥaḍrat **رَحْمَةُ اللهِ تَعَالَى عَلَيْهِ**, Amīr-e-Ahl-e-Sunnat **دَامَتْ بَرَكَاتُهُمُ الْعَالِيَةَ** na vya wanavyuoni wengine waislamu ambavyo huchapishwa na Maktaba-tul-Madīnah vimeshawafikia watu wengi. Vitabu hivi vinasambazwa na hueneza mafunzo ya sunah.

اَلْحَمْدُ لِلّٰهِ عَزَّوَجَلَّ! Dawat-e-Islami ina kitengo cha uchapishaji pia. Juu ya hayo, kaseti na CD nyingi kuhusu bayana za sunnah na

Madanī Muzākaraḥ zimefikia na zinaendelea kufikia kila sehemu ya dunia.

Al-Madīna-tul-‘Ilmiyyāḥ

Majlis ‘Al-Madīna-tul-‘Ilmiyyāḥ’ ina maulamaa (wanavyuoni) na mamufti wa Dawat-e-Islami. Majlis imechukua jukumu la kutuo huduma ya dini katika Sayansi ya kiislamu, utafiti na uchapishaji. Ina idara sita zifuatazo:

1. Shu’baḥ Kutub A’lā Ḥaḍrat (Idara ya vitabu vya A’lā Ḥaḍrat رَحْمَةُ اللَّهِ تَعَالَى عَلَيْهِ)
2. Shu’baḥ Darsī Kutub (Idara ya vitabu vya mtaala)
3. Shu’baḥ Iṣlāḥī Kutub (Idara ya vitabu vya ulinganizi)
4. Shu’baḥ Taftīsh-e-Kutub (Idara ya uhakiki wa vitabu)
5. Shu’baḥ Takhrīj (Idara ya marejeo ya manukuu)
6. Shu’baḥ Tarājim Kutub (Idara ya tafsiri ya vitabu)

Jukumu kuu la Al-Madīna-tul-‘Ilmiyyāḥ’s ni kuvieneza vitabu vya thamani kubwa vya A’lā Ḥaḍrat, Imām-e-Aḥl-e-Sunnat, Imām Aḥmad Razā Khān عَلَيْهِ رَحْمَةُ الرَّحْمَنِ kwa njia nyepesi ya kueleweka kulingana na mahitaji ya sasa.

Majlis-e-Taftish Kutub-o-Rasāil

Waislamu wanaingiwa na hamu ya kusoma vitabu vya dini kila kazi ya Dawat-e-Islami inapopiga hatua. Kulikuwa na wakati ambapo hata vitabu 20 au 30 vilivyoandikwa na wanavyuoni wa Aĥl-e-Sunnat viliweza kuuzika katika mkusanyiko wa kidini lakini sasa, **اَلْحَمْدُ لِلّٰهِ عَزَّوَجَلَّ**, maelfu ya vitabu vinauzwa. Maduka mapya ya kuuza vitabu vya kiislamu yanafunguliwa na waandishi wapya wanachapishiwa machapisho yao.

Mfumo wa biashara ni kwamba ikiwa mahitaji ya bidhaa yataongezeka, watengezaji watalenga kuiongeza idadi ili wapate mapato zaidi badala ya kuhifadhi ubora wa bidhaa. Hali hii ilidhihirika kwa vitabu. Mfumo wa kuuza vitabu vilivyojaa makosa tele ulienea kwa haraka mno. Ili kuzuia hali ya hatari, waislamu wenye maduka ya vitabu, waandishi wapya na watungaji, walialikwa katika Madanī Mashwarāh, ili kuwatahadharisha kuhusu hatari ya kupata dhambi kutokana na kuchapisha na kusambaza upotofu kuhusu mafunzo ya kiislamu kupitia vitabu visivyo na uthabiti. Jambo hili liliwaathiri pakubwa. Kwa hivyo, ili kuzuia kusambaa kwa mafunzo potofu ya kiislamu miongoni mwa waislamu na kupata dhambi kutokana na kuchapisha vitabu ambavyo si thabiti, ‘Majlis-e-Taftish-e-Kutub-o-Rasāil’ (Idara ya kuhakiki vitabu na vijitabu) imeanzishwa. Majlis hii hupitia maandishi mbali mbali na ili kuzuia makosa ya imani, kufuru, uadilifu, sarufi ya kiarabu na hukumu za sharia na kutoa cheti cha uthibitisho baadaye.

Kozi Mbalimbali

Kozi mbali mbali hutolewa ili kuwapa mafunzo walinganizi. Kwa mfano kozi ya Madanī Qāfilāh na Madanī In'āmāt ya siku 41, kozi ya Tarbiyyat ya siku 63, Kozi ya Imāmat, kozi ya Mudarris na kadhalika. Walinganizi wanafunzwa lugha ya ishara kupitia kozi ya siku 30 ya Qufl-e-Madīnah ili kulingania watu (vipofu, viziwi na mabubu) katika njia ya haki. Walinganizi wanawezeshwa kuzungumza, kutoa bayana, kutoa Qasida na kufanya Żikr na kutoa Du'a kwa lugha ya ishara.

Īṣāl-e-Šawāb

Kwa ajili ya Īṣāl-e-Šawāb (kufanya jambo jema kwa niya ya kumfikishia marehemu thawabu), Maktaba-tul-Madīnah hutoa nafasi ya kuchapisha jina la yule anayekusudiwa na familia yake katika vitabu kama Faizān-e-Sunnat, Laws of Ṣalāh, Ṣalāh of Islamic Sisters na vinginevyo.

Viduka vya Maktaba-tul-Madīnah

Maktaba-tul-Madīnah inatoa huduma na vifaa vya kuweka viduka vya kugawanya vitabu na vijitabu katika matanga, sherehe za harusi nakadhalika. Ukiwasiliana nao, mipango yote itafanywa na wahusika wa Maktaba.

صَلَّى اللّٰهُ تَعَالَى عَلَى مُحَمَّدٍ

صَلُّوا عَلَى الْحَبِيبِ

Majlis-e-Tarājim

Vitabu na vijitabu vinavyochapishwa na Maktaba-tul-Madīnah vinatafsiriwa kwa lugha mbali mbali na Majlis-e-Tarājim.

اَلْحَمْدُ لِلّٰهِ عَزَّوَجَلَّ mpaka sasa vimeshatafsiriwa kwa lugha 27 za ulimwenguni. Nazo ni:

- | | | |
|----------------|----------------|---------------|
| 1. Kiarabu | 2. Kiingereza | 3. Kifaransa |
| 4. Kispanshi | 5. Kirusi | 6. Kinowiji |
| 7. Kidenishi | 8. Kichina | 9. Kitaliano |
| 10. Kijarumani | 11. Kireno | 12. Kimalayi |
| 13. Kituruki | 14. Kigiriki | 15. Kikrioli |
| 16. Kibengali | 17. Kitelugu | 18. Kitamili |
| 19. Kikanada | 20. Kihausa | 21. Kiswahili |
| 22. Kihindi | 23. Kigujarati | 24. Kisinjala |
| 25. Kifursi | 26. Kisindhi | 27. Kipashto |

Ijtimāi Ng'ambo

Katika nchi mbalimbali Ijtimai za siku mbili zinafanyika na huhudhuriwa na maelfu ya wakazi waislamu. Kutokana na karama za Ijtimāi hizi, mara kwa mara makafiri husilimu na mwisho wa Ijtimāi hizi, Madanī Qāfilah husafiri katika njia ya Allah عَزَّوَجَلَّ

Tarbiyyati Ijtimai

Tarbiyyati Ijtimai zinafanywa kwa ajili ya ndugu waislamu wasimamizi ndani na nje ya Pakistan kwa siku mbili au tatu. Maelfu ya ndugu waislamu huhudhuria na hupewa muongozo kamili wa usimamizi wa kazi za Madani ya Dawat-e-Islami nawanarudi (kwao) na ari mpya.

Madrasa-tul-Madīnah Katika mtandao

اللَّحْمَدُ لِلَّهِ عَزَّوَجَلَّ Majlis ‘Madrasa-tul-Madīnah katika Mtandao’ ilianzishwa katika mwezi wa Shawwal-ul-Mukarram 1432 A.H. (Septemba, 2011). Inatoa huduma ya mafunzo ya kusoma Qur’an kwa njia sahihi kwa waislamu kutoka nchi mbalimbali kwa kutumia mtandao bila malipo yoyote. Mbali na kusoma Qur’an kwa usahihi, ndugu waislamu wanafunzwa hukumu za kimsingi za Kiislamu kama vile Wuḍhu, Ghusl, Tayammam, Adhan, Ṣala, Zaka, Kufunga, Hajj na kadhalika.

Dār-ul-Madīnah

اللَّحْمَدُ لِلَّهِ عَزَّوَجَلَّ! Idara nyingine muhimu iitwayo Dār-ul-Madīnah ilianzishwa tarehe 25th Ṣafar-ul-Muzaffar 1432 A.H. (31 Januari 2011). Lengo la idara hii ni kuelimisha kizazi kipya cha waislamu kuhusu elimu ya dini na dunia kwa pamoja na

kuwalea ili waishi maisha yao wakifuata sunnah za Bwana wetu Mtume صَلَّى اللهُ تَعَالَى عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ.

صَلُّوا عَلَى الْحَبِيبِ صَلَّى اللهُ تَعَالَى عَلَى مُحَمَّدٍ

Madani Chaneli

Iwapo anayeabudu moto atafunguwa hoteli katika makazi ya waislamu, itakuwa vigumu kumshawishi kila mtu kuwa kula nyama au vyakula vilivyopikwa kwa nyama katika hoteli hii ni haramu. Njia bora ni muislamu naye afungue hoteli katika sehemu ile ile hapo basi itakuwa rahisi kuwashawishi waislamu kula katika hoteli ya muislamu mwenzao. Hali hii ni sawa na televisheni ambayo wakati huu inapatikana karibu kila nyumba. Kila muislamu mwenye busara anatambua uovu unaosambazwa na televisheni katika jamii yetu. Ingawa walinganizi wa Dawat-e-Islami walijitahidi kuondoa televisheni katika jamii, hawakufaulu kama ilivyotakikana.

Kwa vile watu wengi wanavutiwa sana kutazama televisheni na hawawezi kujizuia ingawa wanayajua madhara yake katika maisha yao ya dunia na ya akhera. Mbali na kuchafuliwa tabia zao shetani pia anaharibu desturi na maadili yao ya kiislamu. Wanaopinga uislamu wanafanya vitimbi kugeuza mafunzo ya kiislamu kwa kusingizia 'Uislamu wa kisasa'. Hali hii hupunguza nguvu imani halisi katika nyoyo za waislamu.

Ikiwa tutashutumu utazamaji wa televisheni misikitini, hatutarajii kupata mabadiliko makubwa kwa sababu asilimia tano tu ya waislamu ndiwo ambao huhudhuria sala misikitini. Na zaidi, waislamu wengi wanaosali misikitini huwa hawana hamu ya kusikiliza mahubiri ya dini. Aidha, nani atawafikishia ujumbe kina dada? Na iwapo tutachapisha vitabu na vijitabu vya dini, ni waislamu wachache tu ndio ambao wanahamu ya kuvisoma. Katika hali kama hii ya kusikitisha, juhudi zetu za kuubadilisha umma wa kiislamu zikibakia tu misikitini na katika ijtimai na kadhalika, hatutaweza kuufikisha ujumbe wetu kwa waislamu wengi. Kwa upande mwingine maadui wa uislamu wako mbioni daima kuwashawishi na kuwapotosha waislamu kwa kuwapa habari potofu zisizo za kweli kupitia idhaa zao potofu za televisheni.

Kwa hivyo tumegundua kuwa haiwezekani kukomesha athari mbaya ya idhaa za televisheni za aina hii katika jamii. Tumbakishwa na njia moja tu ya kutumia televisheni kusambaza mafundisho ya uislamu huku tukijaribu kuwaamsha waislamu kutoka katika ujinga na kuwatanabahisha kuhusu madhara ya dhambi na juu ya mafunzo ya dini ya kiislamu yaliyopotoshwa. Hali hii inaweza kufananishwa na mafuriko. Maji yanaweza kuelekezwa mashambani ili yasiharibu nyumba. Wakati huo huo maji haya yanasaidia kunyunyuzia mimea. Kwa hivyo tulipojua kwamba yawezekana kudhihirisha idhaa ya televisheni ya kiislamu ili kuwapa waislamu mafunzo ya kweli ya kiislamu bila kuwepo na sinema, nyimbo, ngoma na vioja vyo vyote vyenye

dhambi, Markazī Majlis-e-Shūrā ya Dawat-e-Islami wakafanya bidii na wakaanzisha Idhaa ya Madanī katika mwezi Mtukufu wa Ramadhan, 1429 A.H. (2008). Idhaa ya Madanī inapitisha habari katika majumba ya waislamu kuhusu Sunna na wamefaulu pakubwa kwa muda mfupi mno!

Ni wazi kuwa waislamu watakuwa salama kutokana na idhaa za televisheni zenye kuonyesha mambo ya dhambi madamu watatazama vipindi vya Idhaa ya Madani. Kwa rehema ya Allah ﷺ, Idhaa ya Madanī imefaulu zaidi kuliko tulivyotarajia. Tunapokea ujumbe mwingi kila siku wakatupongeza na kutupa moyo kutoka ulimwengu mzima. Mbali na pongezi, jumbe hizi zimetoa taarifa kuhusu mabadiliko makubwa mazuri katika maisha ya watu wengi kwa ajili ya kutazama Idhaa ya Madani. Watu wengi wametubia, wameanza kusali na kuanza kufuata Sunnaḥ. Vifuatavyo ni visa vitatu vinavyoonyesha kufaulu kwa Idhaa ya Madani:

1. Asiyekuwa Muislamu, anaukubali Uislamu

Ndugu muislamu kutoka Markaz-ul-Auliyā (Lahore) aliripoti kuwa katika karakana iliyokuwa katika eneo lao, walikuwa na televisheni. Wafanyikazi walikuwa wakitazama idhaa mbalimbali katika televisheni. Ilipofunguliwa Idhaa ya Madani katika mwezi mtukufu wa Ramadhan, 1429 A.H. (2008), walivutiwa zaidi na vipindi vyake na wakaanza kutazama kila siku. Mmoja wa wafanyikazi hawa alikuwa mkristo. Alivutiwa sana na vipindi vya

Idhaa ya Madani. **اَلْحَمْدُ لِلّٰهِ عَزَّوَجَلَّ** Aliathiriwa zaidi na unyenyekevu wa Amīr-e-Aḥl-e-Sunnat **دَامَتْ بَرَكَاتُهُمُ الْعَالِيَةَ** na baada ya siku tatu tu akapiga Shahada na akawa muislamu.

صَلُّوْا عَلٰى الْحَبِيْبِ صَلَّى اللّٰهُ تَعَالٰى عَلٰى مُحَمَّدٍ

2. Sasa naona aibu kutazama idhaa zenye kuonyesha uchafu

Mlinganizi wa kike wa Dawat-e-Islami alieleza kuwa dada mmoja muislamu, watoto wake pamoja na baba yao walikuwa na hamu kubwa kutazama idhaa zenye kuonyesha uchafu. Televisheni iliyokuwa ikionyesha vipindi vya wanawake waliokuwa wakicheza ngoma wakiwa uchi, iliwashwa kuanzia asubuhi. Watoto pia walitazama vipindi hivi punde tu, waliporegea kutoka shuleni.

اَلْحَمْدُ لِلّٰهِ عَزَّوَجَلَّ Mwezi Mtukufu wa Ramadhan (1429 A.H, 2008) ulipofika, Baraka kubwa iliyotokea ni kufunguliwa kwa Idhaa ya Madani. Idhaa hii iliwafurahisha sana wapenzi wa Mtume **صَلَّى اللّٰهُ تَعَالٰى عَلَيْهِ وَاٰلِهٖ وَسَلَّمَ**.

اَلْحَمْدُ لِلّٰهِ عَزَّوَجَلَّ ! Katika nyumba hii ya dada wa kiislamu ambapo zamani walikuwa wakitazama idhaa zinazoonyesha vipindi vichafu kila wakati, sasa wanatazama vipindi vya Idhaa ya Madani peke yake. Mtu yeyote akifungua idhaa ambayo inaonyesha mambo ya uchafu, kwa haraka huibadilisha kwa idhaa ya Madani. Mumewe asema, “Naona aibu kutazama idhaa

zinazoonyesha mambo machafu kwa sababu mimi ni mfuasi wa Amīr-e-Ahl-e-Sunnat دَامَتْ بَرَكَاتُهُمُ الْعَالِيَةِ Naye anaonyeshwa katika idhaa ya Madani. Vipi mimi nitazame idhaa zinazoonyesha vipindi vya aibu?

صَلُّوا عَلَى الْحَبِيبِ صَلَّى اللَّهُ تَعَالَى عَلَى مُحَمَّدٍ

3. Baa ilifungwa

Ndugu muislamu kutoka Markaz-ul-Auliya (Lahore) alieleza kwamba, kulikuwa na mtu mmoja akifanya biashara ya kuuza pombe, na kuonyesha sinema za ngono katika baa yake. Baada ya kutazama vipindi vya idhaa ya Madani alivutiwa mno na vipindi vya idhaa hii hadi akaamua kuifunga baa yake kwa siku mbili tu.

صَلُّوا عَلَى الْحَبِيبِ صَلَّى اللَّهُ تَعَالَى عَلَى مُحَمَّدٍ

Tanbihi: Ili usome visa zaidi kama hivyo vya Baraka za Idhaa ya Madani, soma kijitabu cha ‘*A non-Muslim embraces Islam*’ kilichochapishwa na Maktaba-tul-Madinah.

Maua 8 ya Madani ya Dawat-e-Islami

Kutoka kwa: Shaykh-e-Tariqat, Amīr-e-Ahl-e-Sunnat, ‘Allāmah Maulānā Abu Bilal Muhammad Ilyas Attar Qadiri Razavi دَامَتْ بَرَكَاتُهُمُ الْعَالِيَةِ

1. Lengo la kimsingi la Dawat-e-Islami ni kueneza mafunzo ya kiislamu ulimwengu mzima kwa njia ambayo kwamba walinganizi wa kiislamu wenyewe washikamane na Sunna na kuwaachia ‘mijadala’ wanavyuoni wa Aĥl-e-Sunnat ambao ni wajuzi wa mambo hayo.
2. Mafunzo ya kiislamu haya yanarejelea maneno na vitendo vya kipenzi chetu Mtume aliyebarikiwa صَلَّى اللهُ تَعَالَى عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ ambavyo vilifuatwa kwa dhati na Sayyiduna Imām Abū Ḥanīfah, Sayyidunā Imām Mālik, Sayyidunā Imām Shāfi’ī na Sayyidunā Imām Aĥmad Bin Ḥanbal رَضِيَ اللهُ تَعَالَى عَنْهُمْ, ambavyo vilisambazwa na Sayyidunā Imām Abul Ḥasan Ash’arī na Sayyidunā Imām Abū Manṣūr Maturīdī رَضِيَ اللهُ تَعَالَى عَنْهُمَا, na ambavyo vilitekelezwa na mfalme wa Baghdad - Ghauš Pāk, Sayyidunā Shaykh ‘Abdul Qādir Jīlānī, Gharīb Nawāz Sayyidunā Khuwājāh Mu’in-ul-Ḥaq Waddīn Chishti, Sayyidunā Shaykh Shahāb-ul-Ḥaq Waddīn Suĥarwardī na Sayyidunā Shaykh Bahā-ul-Ḥaq Waddīn Naqshbandī رَضِيَ اللهُ تَعَالَى عَنْهُمْ, ambavyo vilikubalika na wanavyuoni wa Aĥl-e-Sunnat, kwa mfano, muandishi wa ‘Rad-dul-Muĥtār’, Khātīm-ul-Fuqāhā, Sayyidunā Shaykh Sayyid Muhammad Amīnuddīn Ibn ‘Ābidīn Shāmī مُحَمَّدِيسْ سَيِّدُ السَّامِيِّ, Sayyidunā Shāh Mullā Jīwan Ḥīndī عَلَيْهِ رَحْمَةُ الْقَوِيِّ, Sayyidunā Shāh ‘Abdul ‘Azīz Muĥaddīš Dīhlvī عَلَيْهِ رَحْمَةُ الْقَوِيِّ na wengine wengi hususan akiwemo A’lā Ḥaḍrat, Imām wa Aĥl-e-Sunnat, mkomeshaji wa Bid’ah, Mujaddid wa Ummaĥ, mfufuzi wa Sunnah, mwanachuoni wa Sharī’ah, kiongozi wa

Ṭarīqah, ‘Allāmah, Maulānā, Al-Ḥāj Al-Ḥāfiẓ, Al-Qārī Ash-Shāh Imām Aḥmad Razā Khān رَحْمَةُ الرَّحْمٰن عَلَيْهِ وَسَلَّمَ ambaye amefafanua mafunzo ya wanavyuoni hao wa kiislamu katika vitabu vyake vyenye manufaa kama vile ‘Al-Mu’tamad-ul-Mustanad’, ‘Tamhīd-ul-Īmān’, ‘Ḥussām -ul -Ḥaramayn’ nk.

3. Waislamu wote, wa kike na wa kiume, sharti washikamane na mafunzo ya A’lā Ḥaḍrat رَضِيَ اللهُ تَعَالَى عَنْهُ. Mafunzo ya A’lā Ḥaḍrat ni sawa na ya maswahaba wa Mtume صَلَّى اللهُ تَعَالَى عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ na wema waliotangulia, yaani, kuamini upweke wa Allah عَزَّوَجَلَّ na kumwabudu yeye peke yake, na kumwamini Mtume Muhammad صَلَّى اللهُ تَعَالَى عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ kuwa ni mtume wa kweli na wa mwisho aliyeletwa na Allah عَزَّوَجَلَّ. Vile vile kuwa nayo moyoni mapenzi na taadhima kwa Allah عَزَّوَجَلَّ na Mtume wake صَلَّى اللهُ تَعَالَى عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ, bila kupinga mambo ya wajib katika imani, kuepukana na kumkufuru Allah عَزَّوَجَلَّ, kumkosea heshima Mtume صَلَّى اللهُ تَعَالَى عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ na maswahaba wake رَضِيَ اللهُ تَعَالَى عَنْهُمْ nk. na kuepukana na wanaokufuru na wakosefu wa adabu.
4. Katika Uislamu wanavyuoni wa kweli wanautukufu na heshima zaidi ya waislamu wengine kwa ajili ya elimu ya dini waliyonayo. Katika kufanya ibada, mwanachuoni wa kiislamu hupata thawabu zaidi kuliko mwislamu mwingine asiyemwanachuoni. Sayyidunā Muhammad Ibn ‘Alī رَضِيَ اللهُ تَعَالَى عَنْهُمَا ameeleza kuwa, ‘rakaa 2 zinazoswaliwa na mwanachuoni ni bora mara 70 ya rakaa 2 zinazoswaliwa na asiyekuwa mwanachuoni’. (*Kanz-ul-‘Ummāl, vol. 10, uk. 87*)

Kwa hivyo ni muhimu kwa wale wote wanaohusiana na Dawat-e-Islami na kila muislamu kutohitilafiana na wanavyuoni wa Aĥl-e-Sunna. Usiache kuwaheshimu na kuwatukuza. Jiepushe na kuwadharau kabisa. Usiwasengenye, usiwaumbue tabia zao na matendo yao bila ya ruhusa ya Sharia. Matendo hayo ni dhambi kubwa na haramu yanayomtia mtu motoni. Sayyidunā Abul Ḥaḥṣ-*ul-Kabīr* عَلَيْهِ رَحْمَةُ الْقَدِيرِ ameeleza, ‘Yule anayemsengenya mwanachuoni (atafufuliwa) siku ya kiyama (katika hali ambayo) itaandikwa katika uso wake; mtu huyu amekata tamaa na Rehema ya Allah عَزَّوَجَلَّ.’ (*Mukāshafa-tul-Qulūb, fi Bayān al-Ghībah*, pp. 71)

Sayyidunā Abu Ḥar Ghifārī رَحْمَى اللَّهِ تَعَالَى عَنْهُ ameeleza, ‘Mwanachuoni ni dalili na ushahidi wa Allah عَزَّوَجَلَّ ulimwenguni; yeyote anayemuumbua, ameangamia.’ (*Kanz-ul-‘Ummāl, vol. 10, pp. 77*)

A’lā Ḥaḥḍrat Imām Aḥmad Raza Khān عَلَيْهِ رَحْمَةُ الرَّحْمَنِ ameeleza, ‘Kumkashifu mwanachuoni na kumpinga ni Ḥarām. Ni hasara kwa muislamu kujitenga na mwanachuoni pamoja na kukataa mafunzo yake ya dini. (*Fatawa Razaviyyah, vol. 23, pp. 711*) Wale wajinga wasio na busara ambao huwatusi wanavyuoni kwa kusema: ‘Tahadhari naye ndugu! Huyu ni ‘shehe’, ‘mashehe ni walafi’, ‘wanatuonea wivu’, ‘hakuna anayewasikiliza’, ‘Muache! Yeye ni ustadhi’, مَعَاذَ اللَّهِ عَزَّوَجَلَّ watu wengine huwaita wanavyuoni kwa dharau ‘Hawa maustadhi’ nk: watu kama hawa wanafaa kuogopa.

Katika kueleza hukumu tofauti tofauti katika sharia za kumvunjia heshima mwanachuoni, A'lā Ḥadrat رَحْمَةُ اللهِ تَعَالَى عَلَيْهِ ameleeza, 'Iwapo mtu atamzungumza mwanachuoni vibaya kwa sababu ni mwanachuoni, basi hii ni kufuru. Ikiwa ataitakidi kuwa ni wajibu kumuheshimu mwanachuoni kwa sababu ya elimu yake ya dini lakini amzungumze vibaya au amtukane au amdharau kwa sababu ya chuki za kibinafsi, basi yeye ni Fāsik mkubwa na Fājir [mtenda dhambi]. Ikiwa amemuwekea chuki mwanachuoni bila sababu basi ni 'mgonjwa wa moyo' na mwenye roho chafu na kuna hatari ya kukufuru.

Imeelezwa katika 'Khulaswa': مَنْ أَبْغَضَ عَالِمًا مِنْ غَيْرِ سَبَبٍ ظَاهِرٍ خِيفَ عَلَيْهِ الْكُفْرُ: (Mwenye kumwekea chuki mwanachuoni bila sababu yuko katika hatari ya kukufuru). (*Fatawa Razaviyyah, vol. 10, pp. 140*)

Maneno na matendo yafuatayo ni mifano ya kuonyesha dharau kwa Sharia na wanavyuoni wa kiislamu. مَعَادَ اللهِ عَزَّوَجَلَّ Iwapo mtu atamvunjia heshima mwanachuoni kwa aidha maneno au matendo yafuatayo kwa sababu ya elimu yake ya dini basi mtu huyo ni sharti atubie na airudie tena imani yake. Ikiwa ameo basi airudie tena nikaha yake (ndoa). Zaidi ya hayo ikiwa alikuwa Murīd basi pia arudie Ba'at kwa sababu maneno na matendo haya yanamsababisha mtu kutoka katika uislamu.

- ❖ Kukashifu Sharia ya kiislamu ni kufuru. Kwa mfano ikiwa mmoja atasema, "Potelea mbali na Sharia", atakuwa kāfiri. Vile vile ikiwa fatwa kutoka kwa mwanachuoni anayetegemewa, amepewa mtu na akasema, "Mimi fatwa

fatwa hizi siziamini.” Basi mtu huyo atakuwa kafiri. (*Taken from Bahār-e-Sharī‘at, part 9, pp. 172*)

- ❖ “Hawa Mashehe wajua nini?” Kufuru yajitokeza wazi wazi katika sentensi hii. Kuwadharau wanavyuoni ni kufuru. (*Fatawa Razaviyyah, vol. 6, pp. 24*)
- ❖ Ikiwa mtu atasema, “Mashehe wote ni wahuni.” Yaani akikusudia wanavyuoni wote basi ni kufuru pia. (*Fatawa Amjadiyyah, vol. 4, pp. 454*)
- ❖ “Wanavyuoni hawa wamechafua nchi” – Uneni huu ni kufuru. (*Taken from Fatawa Razaviyyah, vol. 6, pp. 115*)
- ❖ Ni kufuru pia kusema Mashehe wamevunja vunja dini.
- ❖ Kusema, “Allah عَزَّوَجَلَّ ameiteremsha dini ikiwa rahisi, lakini mashehe wameifanya iwe ngumu” ni kufuru kwani **الْإِسْتِحْقَافُ بِالْأَشْرَافِ وَالْعُلَمَاءِ كُفْرٌ** (i.e. kuwadharau wanavyuoni na kizazi cha Mtume ni kufuru). (*Majma’-ul-Anhar, vol. 2, pp. 509*)
- ❖ Iwapo mtu atasema, “Elimu wanayofundisha wanavyuoni ni ngano na hadithi.” Ama “...ni mataminio” au “...ni uongo.” Au akisema, “Siamini elimu udanganyifu”, yaani anamaanisha kuwa Sharia ni udanganyifu, uneni huu wote ni kufuru. (*Fatawa ‘Alamgīrī, vol. 2, pp. 270*)
- ❖ Ikiwa mtu atasema, “Itanifaa nini elimu ya dini ya kiislamu? Mtu ni bora awe na pesa mfukoni mwake!” Mtu kama huyu anahukumikiwa kuwa amekufuru.

- ❖ Iwapo mtu atamwambia mwanachuoni, “Usituletee elimu yako hapa, kaa nayo mwenyewe na uihifadhi chunguni.” Kusema hivi ni kufuru. (*Fatawa ‘Alamgīrī, vol. 2, pp. 271*)

Kumbuka! Wanavyuoni wa Aĥl-e-Sunnat tu wana stahili kuheshimiwa. Aidha kuhusu wanachuoni wapotofu, mtu afaa awaepuke. Ni haramu na ni sumu kwa imani ya muislamu kuwaheshimu, kusikiza hutuba zao, kutwalii vitabu vyao na kuwa pamoja nao.

5. Desturi za Aĥl-e-Sunnat ni utambulisho wetu. Kwa hivyo musifanye uvivu kufuata desturi hizi. Kwa mfano:

- a) Katika mwezi wa Rabi’-un-Nūr, sherehekeeni kuzaliwa kwa Mtume صَلَّى اللهُ تَعَالَى عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ. Pambeni nyumba zenu, maduka, magari, misikiti na mitaa kwa taa za kumetameta na bendera za kijani katika siku 12 za mwanzo au mwezi mzima.

Utumieni usiku wa kuzaliwa Mtume صَلَّى اللهُ تَعَالَى عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ (yaani. tarehe 12th ya Rabi’-un-Nūr) katika Ijtimai ya Żikr-o-Na’at (dhikri na qasida) na mukaribishe ‘Asubuhi ya Rehema’ kwa kusimama na bendera ya kijani mikononi huku mukimsalia Mtume صَلَّى اللهُ تَعَالَى عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ siku ya 12 Rabi’-un-Nūr, yaani Siku ya kuzaliwa Mtume صَلَّى اللهُ تَعَالَى عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ. Pia fanyeni au shirikieni katika zefe za Maulidi.

- b) Pangeni Ijtimai’ ya Żikr-o-Na’at usiku wa Miraj, siku za makhalifa wanne wa mwanzo wa uislamu, sherehe ya

kila mwaka ya Giyārḥwīn na siku ya Razā (25 Safar-ul-Muẓaffar).

- c) Siku za ‘Urs’ (hawli za mawalii), pageni Madanī Qāfilāḥ katika misikiti iliyokaribu na maeneo ambayo hawli ya walii inafanyika na mulinganie watu katika haki kulingana na ratiba ya Madanī Qāfilah, ili mupate baraka nyingi za mawalii hao.
6. Wale wote ambao wana uhusiano na Dawat-e-Islami wafanye kazi za Madani za Dawat-e-Islami na watii Markazī Majlis-e-Shūrā, Intizāmī Kābīnāḥ ya nchi zao, Majlis-e-Mushāwarat ya sehemu zao na hata Žāilī Nigrān wa Mushāwarat ya maeneo yao. Kutii huku kuwe ni katika mambo yaliofungamana na sharia.
7. Shetani hufanya uhuharibifu mkubwa katika kazi za dini kwa kusababisha watu kusengenyana. Hivyo basi ukipata ubaya au kasoro kwa nduguyo mwislamu, usimsengenyeye kwa kumtolea aibu zake bila ya ruhusa ya sharia. Badala yake, ikiwezekana, mrekebishe mukiwa faraghani. Ikiwa hili halikusaidia, basi nyamaza na umuombee Mola (amrekebishe).

Ikiwa kutakuwa na hofu kwamba jambo hili litaleta hasara katika kazi ya dini, basi tafuta ushauri kwa Žāilī Nigrān wa Mushāwarat yako. Aidha uzungumze naye faraghani au umwandikie. Bora tu aweze kulitatua tatizo. Iwapo atashindwa, bado ukiongozwa na sharia, lipeleke tatizo hili

kwa Ḥalqah Nigrān wa Mushāwarat yenu. Akishindwa, basi hatua kwa hatua lipeleke kwa Nigrān wa ‘Alāqāi Mushāwarat, halafu kwa Nigrān wa Mushāwarat wa mji wenu, halafu kwa Nigrān wa Mushāwarat wa tarafa yenu na halafu kwa Nigrān wa Intizāmī Kābīnah wa nchi yenu.

Kumbuka! Bila ya ruhusa ya sharia, ukitaja uovu wa muislamu hata kama ni kwa msimamizi mkubwa kiasi gani, utakuwa ni mtenda dhambi. Zaidi ya hayo, habari ikisambaa kwa ajili yako na ikasababisha vurugo katika shirika na kupotea kwa kazi za Madani, lawama ya ufisadi katika kazi za dini na kuna uwezekano wa kupata adhabu kali kesho akhera.

8. Kuna namna mbili za bayana zinazotolewa katika Ijtimai:
 - a) Walinganizi ambao ni weledi wa elimu ya dini na wenye matendo mema (kwa mfano, wale ambao wamepitia Chuo cha Dars-e-Nizāmī na wenye uwezo wa kuhifadhi na kuepuka makosa ya kisharia) wanaruhusiwa kutoa bayana bila kusoma kwenye vitabu (yaani kwa moyo).
 - b) Walinganizi ambao si weledi wa elimu watoe nakala za kurasa kutoka kwa vitabu vya wanavyuoni wa Ahl-e-Sunnat, wazibandike katika madaftari yao na wanapotoa bayana, wasome vile vile ilivyoandikwa.

Ili upate Baraka nyingi duniani na kesho akhera, jiunge na mazingira ya Madani ya Dawat-e-Islami. Hudhuria Ijtimai ya

Sunnah ya kila wiki ya Dawat-e-Islami inayofanyika mjini unamoishi. Funga safari pamoja na Madanī Qāfilah na uendelee kutazama idhaa ya Madani.

صَلُّوا عَلَى الْحَبِيبِ صَلَّى اللَّهُ تَعَالَى عَلَى مُحَمَّدٍ

Idara 63 za Dawat-e-Islami

Huduma za kulingania na kurekebisha watu: Madanī In'āmāt, Madanī Qāfilāh, kuwalingania wasiokuwa waislamu, Majlis Berūn-e-Mulk.(Baraza la nchi za ng'ambo).

Huduma za Jumuiia na Mafunzo: Vituo vya Mafunzo vya Madanī, Ijtimai ya mtaani na ya wiki, Ijtimai ya mkoa na ya kimataifa, Tarbiyyati Ijtimā'āt kwa ndugu waislamu wasimamizi, Ijtimā'i ya ng'ambo, I'tikāf ya pamoja, Majlis Hajj & 'Umrah, Majlis Madanī Mużākarah.

Huduma za Elimu: Jāmi'a-tul-Madīnah (kwa wavulana), Jāmi'a-tul-Madīnah (kwa wasichana), Madrasa-tul-Madīnah, Madrasa-tul-Madīnah (kwa wasichana), Madrasa-tul-Madīnah (kwa watu wazima), Madrasa-tul-Madīnah (kwa kina dada), Madrasa-tul-Madīnah katika mtandao, Dār-ul-Madīnah, Dār-ul-Iftā Ahl-e-Sunnat, Dār-ul-Iftā katika mtandao, Takhaşşuş-fil-Fiqh, Takhaşşuş-fil-Funūn, Majlis Tawqīt, Majlis Tahqīqāt-e-Shar'īyyah na kozi mbali mbali.

Huduma za utafiti na Habari: Majlis Al-Madīna-tul-‘Ilmiyyāh, Majlis Tarājim, Maktaba-tul-Madīnaḥ, Viduka vya Maktaba-tul-Madīnaḥ , Idhaa ya Madanī, Majlis ya Teknoloija ya Habari.

Huduma za Jamii: Majlis Shu’ba-e-Ta’līm, Majlis ya ndugu waislamu mahsusi, Majlis ya Gerezani (Faizān-e-Quran), Majlis kwa wafanyibiashara, Majlis ya wanasheria, Majlis ya Usafiri, Majlis ya madaktari, Majlis ya mahakimu, Majlis ya madaktari wa mifugo, Majlis ya matabibu wa Homopathia, Majlis ya michezo, Majlis ya ‘Ushr’, Majlis ya Rābiṭaḥ, Majlis ya Rābiṭaḥ bil-‘Ulamāḥ Wal-Mashāikh, Majlis ya Mazārāt (maziwara), Majlis ya habari na machapisho, Majlis ya vitongoji.

Huduma ya ustawi wa Jamii: Majlis Khuddām-ul-Masājid, Majlis Āimmaḥ Masājid, Majlis Madanī Āimmaḥ, Majlis Maktūbāt-o-Ta’wīzāt-e-‘Atṭariyyāḥ, Majlis-e-‘Ilāj, Īsāl-e-Šawāb, Majlis ya ugawanyaji wa vijitabu misikitini na Majlis ya kuwatakia waislamu heri na fanaka.

Huduma za utawala: Majlis Māliyāt (fedha), Majlis ya rasilimali, Majlis Ijārah, Majlis ya usalama.

Huduma anuwai: Mageuzi ya kiMadanī miongoni mwa kina dada waislamu.

صَلَّى اللّٰهُ تَعَالَى عَلَى مُحَمَّدٍ

صَلُّوا عَلَى الْحَبِيبِ

Baraka Za Sunnah

اتخذ بـه عروجن Katika mazingira ya Dawat-e-Islami (shirika la harakati ya Quran na Sunnah la kimataifa lisilo jihusisha na siasa) tuna funza na kufundisha Sunnah za Bwana Mtume صلى الله تعالى عليه وآله وسلم. Hudhuria ijtimai ya kila wiki siku ya al-khamis baada ya sala ya magrib inayofanyika katika mji wako. Safiri pamoja na wapenzi wa Mtume صلى الله تعالى عليه وآله وسلم katika Madani Qafilah na uweke azma yakujaza kadi ya zawadi 72 za Madina (Madani In'amaat) na kumkabidhi msimamizi (Zimmedaar) kila mwezi. Kwa Baraka ya kufanya hivi ان شاء الله tutzaweza kushikamana na Sunnah za Bwana Mtume صلى الله تعالى عليه وآله وسلم na tutachukia maasi na tutaweza kulinda imani yetu.

Kila moja aweke azma hii "Ninataka kusuluhisha nafsi yangu na watu wa ulimwengu mzima ان شاء الله عروجن". Kusuluhisha nafsi yangu nita fuata "Madani In'amaat" na kusuluhisha nafsi za watu wa ulimwengu mzima nita safiri katika "Madani Qafilah" ان شاء الله عروجن.

